| | |
|---|---|
| Title | Utamaduni wa Kiswahili : Misingi ya Lugha |
| Author(s) | Isack, Zainabu Kassu |
| Citation | 外国語教育のフロンティア. 2022, 5, p. 247-258 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/87580 |
| rights | |
| Note | |

*Osaka University Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

Osaka University

# Utamaduni wa Kiswahili: Misingi ya Lugha

## Swahili Culture: The Foundation of the Language

ISACK, Zainabu Kassu

**Ikisiri**

Makala hii fupi ni sehemu ya mfululizo wa makala juu ya Utamaduni wa Kiswahili na Utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla. Awamu hii tumekusudia kutolea ufafanuzi Misingi ya Lugha ya Kiswahili. Kama tujuavyo taaluma ya lugha ni uwanja mpana sana. Tukiangalia kwa mtazamo wa kimatumizi, lugha ni nyenzo muhimu ya mawasiliano, na katika mtazamo mpana zaidi lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni wa watu. Lugha hutumika kuwatambulisha au kuwatofautisha watu kulingana na jamii wanamotokea. Kama ukiuliza Mswahili ni nani kwa mfano, jibu mojawapo ni, "mtu anayesema Kiswahili kama lugha yake ya kwanza". Lakini Kiswahili chenyewe ni nini? au Misingi ya lugha hii ni ipi? Makala hii fupi inakusudia basi kutolea ufafanuzi maarifa ya msingi juu ya lugha hiyo japo kwa muhtasari. Maudhui tajwa yanatarajiwa kuwanufaisha wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika kutajirisha maarifa yao na kuziba mwanya wa rejea zinazowalenga kundi hili juu ya lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla wake. Makala hii pia ni sehemu nzuri ya kuanzia, ya kumpa mwanga mtu yeyote mwenye kiu au shauku ya kujua kuhusu lugha hii adhimu ya Kiafrika; Historia yake, asili yake, dhima zake kutoka zamani na sasa na hata kuzamia katika elimu ya nyanja zake za kitaaluma.

Keywords: Lugha, Lugha ya Kiswahili, Utamaduni wa Kiswahili

**Abstract**

This brief article is a continuation of series of articles on Swahili Culture and African Culture at large. This time we aim at giving brief description on the Foundation of the Swahili Language. As we know Language as an academic field is a very broad one. From a functional perspective Language is a basic communication tool and at large a very core aspect of people's culture. Language is essentially one of the key aspects in identifying or differentianting people of a given society. For example if we pose a question who is a "Swahili" person, we will hear a response like "A Swahili is a person whose mother tongue is Kiswahili". But what is this language really? or what are the Foundation of this Language? This article therefore is an attempt to provide a basic knowledge on the language in a nutshell. Such content is aimed to enrich the knowledge on Swahili

Language for both instructors and learners of Swahili as a foreign language and knowledge of African Culture at large. This paper is also a good starting point for anyone who is keen or has interest in learning about this significant African language.

Keywords: Language, Swahili Language, Swahili culture

## 1. Utangulizi

Makala hii imegawanyika katika sehemu 3: Sehemu ya 1 ni **Utangulizi**; ambayo inafafanua mpangilio wa makala na lengo la makala. Sehemu ya 2 inatolea ufafanuzi mambo ya msingi kuhusiana na **Lugha ya Kiswahili** mambo hayo ni pamoja na; historia yake, asili yake, dhima ya lugha hiyo zamani na hata sasa na kutolea ufafanuzi taaluma za msingi katika isimu ya lugha kwa ujumla tukitolea mifano kutoka lugha ya Kiswahili pale inapojuzu. Sehemu ya 3 na ya mwisho ni: **Hitimisho**; nayo inatoa muhtasari wa kazi hii pamoja na nini mwandishi anapendekeza kwa kazi zijazo.

### 1.1 Lengo la Makala

Makala hii fupi inaangazia juu ya Lugha ya Kiswahili chini ya mada, *Utamaduni wa Kiswahili: Misingi ya Lugha*. Tunakusudia kutambulisha na kutolea ufafanuzi wa mambo ya msingi kuhusu Lugha ya Kiswahili japo kwa muhtasari. Kusema kweli tunapozungumzia suala la *Lugha ya Kiswahili*, hii ni bahari pana sana ambayo imepata kuwashughulisha wanazuoni duniani na ina historia ndefu. Vilevile kuna rejea anwai ama zinazogusia ama kuingia kwa undani juu ya nyanja mbalimbali katika lugha husika. Hata hivyo, nyingi ya rejea hizo zimekusudiwa kwa wanagenzi au wazawa wa Kiswahili kama vile wanafunzi wa sekondari na vyuoni, watafiti, au kutajirisha maarifa na kuziba mwanya wa maarifa juu ya mada mbalimbali. Mijadala mingi katika rejea hizo inafanyika katika lugha inayofahamika zaidi miongoni mwa wanazuoni, wakomavu wa lugha na watafiti wa uwanja huo ambao tayari wana maarifa na uelewa mkubwa. Pengo analoliona mwandishi ni rejea zinazowalenga wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, ambao hawana usuli wa kutosha kuhusiana na lugha hiyo. Kundi hili halijazingatiwa vilivyo katika maandishi ya Kiswahili. Hivyo basi, hapa tunakusudia kumpa mwanga mjifunzaji wa aina hiyo maarifa ya msingi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kutimiza azma hii, tutatumia maandiko yaliyopo juu ya mada hizo na kudondoa katika lugha sahili na japo kwa muhtasari mambo muhimu kuhusu Lugha ya Kiswahili kwa kumzingatia mjifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Rejea zinazotumika katika makala hii hasa vitabu, ni zile zinazotumika kwa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari na vyuoni nchini Tanzania, hivyo tunatarajia kuwa maelezo mafupi katika makala hii yatakuwa chachu

na yatamjengea hamasa mwanafunzi mgeni mwenye raghba ya kuzamia kwa undani katika taaluma fulani ya lugha ya Kiswahili na kuzitumia rejea hizo vilivyo kama sehemu ya kuanzia.

Makala hii ni mwendelezo wa jitihada za mwandishi katika kupunguza mwanya wa rejea juu ya vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla zinazowalenga wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Tunaendelea kusisitiza kuwa; mtu anapojifunza lugha ya kigeni anajifunza utamaduni wa lugha husika pia. Hivyo tunahitaji rejea za kutosha zinazoangazia vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla zinazowalenga kundi husika katika maandiko ya Kiswahili. Makala zilizotangulia zenye mwelekeo huu ni pamoja na: *Makuzi na Hataua za Maisha katika Utamduni wa Kiswahili* (Isack 2018:105-118), *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2019:259-269), *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi* (Isack 2020:193-205) na *Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2020:223-233).

## 2. Lugha ya Kiswahili

Katika sehemu hii tutaangalia maana ya lugha kwa ujumla, historia yake, asili yake, dhima ya lugha hiyo zamani na sasa, na mwishowe tutafafanua taaluma za msingi za Isimu ya Lugha tukitolea mifano Lugha ya Kiswahili pale inapojuzu.

### 2.1 Lugha ni nini?

"Lugha ni sehemu muhimu sana katika maisha ya binadamu na katika jamii wanamoishi. Hivyo, kila kulipo na watu huwapo pia lugha. Pengine hii ndiyo sababu baadhi ya majina ya lugha ndiyo pia majina ya jamii na hata mahali au nchi. Mifano ni kama vile Kingereza -Waingereza - Uingereza; Kijerumani - Wajerumani - Ujerumani; Kisomali - Wasomali- Somalia; Kifaransa - Wafaransa - Ufaransa; Burundi - Warundi - Kirundi, na kadhalika" (Mekacha 2000:1).

Kila jamii ina lugha yake ambayo watu wake wanajivunia kama sehemu ya utamaduni na utambulisho wao, na kwa Waswahili, lugha hiyo ni Kiswahili. Popote penye watu pana lugha na hivyo basi ni vigumu kutenganisha lugha na utamaduni wa watu, au tunaweza kusema viwili hivi huathiriana na huakisiana. Mekacha (2000:2) anatoa fasili ya lugha kama,"ni sauti nasibu za binadamu za kusemwa au kuandikwa zinazotumika na watu wa mahali fulani kwa lengo kuu la mawasiliano. Dhima nyingine za lugha ya binadamu ni pamoja na kumfasili mwanadamu (lugha itumiayo maneno hutumiwa na binadamu tu, ikilinganisha na jinsi wanyama au mimea inavyowasiliana). Dhima nyingine ya lugha ya binadamu ni kufikiri, kila alifanyalo mtu hulifikiri kabla au baada ya kulitenda."

Vivyo hivyo kwa mintarafu ya mwelekeo wa makala hii, tusisitize hapa ikiwa mwanafunzi anajifunza lugha fulani, mbali na kujifunza zile stadi za msingi za kusikiliza, kusoma, kusema na kuandika: Mwanafunzi sharti ajibidiishe kujua vipengele vya utamaduni vinavyoambatana na lugha husika. Lengo la msingi la lugha ni mawasiliano, lakini tuweke hoja bayana kwamba; haitoshi kufahamu tu msamiati wa lugha husika au sarufi yake, bila kujua utamaduni unaofungamana na lugha husika katu mawasiliano hayawezi kuwa kamili.

**2.2 Historia Lugha ya Kiswahili**

Kiswahili ni moja ya lugha kubwa za Kiafrika nacho kimepitia michakato, hatua mbalimbali mpaka kuwa na Kiswahili Sanifu tunachokiona na kukitumia leo katika miktadha rasmi. Katika miktadha isiyo rasmi, tuseme hatuna Kiswahili bali viswahili. Kwani kuna tofauti dhahiri za kimsamiati, na kisarufi zenye kuletwa na athari za kilahaja, kijiografia na miktadha mbalimbali ya kimatumizi. Katika sehemu hii basi hatutajikita katika Viswahili au lahaja za Kiswahili, bali tutatalii kwa ufupi historia ya Kiswahili mpaka kupata Kiswahili Sanifu ambacho ndicho kitumikacho kwa maandishi na mawasiliano rasmi na kufunzwa kama somo na kutumika kufundishia mashuleni.

**2.2.1 Kiswahili Sanifu**

*Lugha Sanifu* kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI (2013:501), ni lugha yenye kufuata taratibu au kanuni zilikubaliwa. Kiswahili Sanifu tunachokiona hivi leo ni matokeo ya usanifishaji au usawazishaji wa lahaja teule ya Kiunguja ili kupata lugha moja yenye ulinganifu wa aina fulani. Kabla ya uteuzi wa Kiunguja kama lahaja ya usanifishaji hapakuwa na usawazisho wa aina hii au tuseme hapakuwa na Kiswahili sanifu bali Viswahili; yaani kila jamii ilitumia lahaja zao kulingana na mazingira ya kijiografia na haja ya mawasiliano yao. Mnamo mwaka 1928, nchi zote za Afrika Mashariki; Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar ziliwakilishwa katika mkutano uliofanyika Mombasa. Na Kiunguja kiliteuliwa kama lahaja ya usanifishaji (Mbaabu 2007:19). Mbaabu (kashatajwa) pia anafafanua kwamba Kiunguja kilipata nguvu kutoka na mkutano wa Dar es Salaam uliofanyika mwaka 1925 ambapo Tanganyika na Zanzibar zilikichagua Kiunguja kuwa lahaja sanifu. Na kutoka mwaka 1930 kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliundwa kwa kazi ya usanifishaji.

**2.3 Asili ya Lugha ya Kiswahili**

Asili ya lugha ya Kiswahili ni moja ya maeneo ambayo yamepata kuwashughulisha wataalamu, watafiti na wanazuoni wa uwanja wa lugha kwa ujumla. Na wataalamu hao wametoa nadhariatete kadhaa juu ya asili ya Kiswahili yaani namna gani lugha hii ilivyoanza. Massamba na wenzake

(2012:4) wanataja nadharia tete muhimu 4; Kwanza ni ile inayodai kuwa Kiswahili kimetokana na kiarabu. Pili, Kiswahili kimetokana na mchanganyiko wa Kiarabu na lugha za Kibantu za upwa wa Afrika ya Mashariki. Tatu: Kiswahili ni lugha ya Kibantu iliyoathiriwa sana na Kiarabu na ya nne ni kuwa Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha za Kibantu zilizokuwa Afrika Mashariki na zikaathiriwa sana na Kiarabu katika kukua kwake (Massamba na wenzake 2012:4). Hapa tutazigawanya nadhariatete hizo kuu mbili katika mitazamo miwili; uarabu au ubantu wa lugha ya Kiswahili tukionyesha hoja zinatolewa kwa kila dai na kuunga mkono mtazamo wenye mashiko au nadhariatete inayoelekea kukubalika zaidi.

**2.3.1 Kiswahili ni Kiarabu**

Nadhariatete hii inatueleza kwamba Kiswahili ni lugha yenye asili ya kiarabu, lugha chotara ya Kiarabu ama pijini/krioli. Mtazamo huu kwanza, unahusisha asili Kiswahili na dini ya Kiislamu, na pili umeegemezwa katika wingi wa maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu kwa mfano maneno kama: Alfajiri, asubuhi, asili, imani, dini, asante, shukrani, salama, dhaifu, laumu, tisa, saba, Ijumaa, Alhamisi n.k. Bosha (1993:39) katika kazi yake, <u>Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya</u>, anabainisha kuwa kwa mujibu wa utafiti wake takriban asilimia 44.3% ya msamiati wa Kiswahili ni maneno yenye asili ya Kiarabu.

Hata hivyo mtazamo huu hauna mashiko na hapa tutatoa sababu 4. Mosi, lugha si msamiati tu, kwa maneno mengine msamiati pekee, si kigezo kamili/hautoshi kuamua sifa ya lugha fulani. Pili, kukopa maneno ya lugha nyingine ni kawaida kwa lugha yoyote iliyo hai na inayokua. Kwa mujibu wa Ayers (1987:196), "Zaidi ya asilimia 80 ya Lugha ya Kiingereza inajumuisha maneno ya mkopo" (tafsiri yangu). Nukuu hii imetolewa na Bosha (1993:37). Bosha (kashatajwa) anaongezea kwa kusema kuwa, "Lakini lugha hiyo inabaki kuitwa Kiingereza na si Kilatini au Kifaransa na bado inaendelea kukopa maneno ya lugha nyingine" (tafsiri yangu). Vilevile, Kiswahili kimekopa maneno katika lugha nyingine pia k.v Kiingereza mf. maneno kama; hospitali, shati, sketi, daktari, Kihindi kwa mfano maneno; laki, biriani, na Kijerumani mfano ni neno; shule. Tatu, uhusiano wa Waswahili na Waarabu ni wa kihistoria. Kutokana na shughuli za biashara na utawala Waarabu walikaa na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki kwa muda mrefu sana. Kwa hivyo si jambo la kustaajabia kama msamiati wa Kiswahili una taathira kubwa kutoka katika Kiarabu. Jambo hili linaakisiwa na wingi wa maneno ya mkopo katika nyanja za biashara, utawala na dini kwa mujibu wa Bosha (1993:33). Nne, kunasibisha asili ya lugha na dini ni sababu dhaifu sana, kwani kama asemavyo Masamba na wenzake (2012:6), "Lugha haiwi lugha kwa sababu ya imani. Hata hiyo lugha ya Kiarabu yenyewe ilikuwapo karne nyingi kabla ya majilio ya Uislamu". Hivyo basi, ni muhimu kutenganisha mambo haya mawili wazi.

### 2.3.2 Kiswahili ni Kibantu

Hii ndiyo nadhariatete au mtazamo unaoelekea kukubalika zaidi kwa kuzingatia ukweli kuwa vigezo vya ubainishaji wa lugha katika makundi maalum duniani ni vipengele vya Kiisimu kama; msamiati wa msingi, fonolojia, mofolojia na sintaksia. Na ushahidi wa Kiisimu unatuonyesha kuwa sarufi ya Kiswahili kwa kila kiwango inafuata kanuni na taratibu za lugha nyingine za Kibantu. Taratibu hizo hudhihirika kwa mfano katika muundo wa silabi na kanuni za kuunda maneno ya lugha, mpangilio na sifa za viambajengo katika sentensi, na kushabihiana kwa mizizi ya msamiati wa msingi kama vile maneno yatajayo sehemu za mwili au maumbile ya asili.

Zaidi, ni vizuri kutaja kuwa nchini Tanzania, Kiswahili si lugha pekee au lugha mama kwa wazawa walio wengi wa nchi hiyo. Kuna lugha za kienyeji zaidi ya 120 nchini humo. Hata hivyo, Kiswahili kinabaki kuwa lugha adhimu na chenye hadhi na dhima nyeti kama inavyofafanuliwa katika sehemu ya 2.4.

### 2.4 Dhima ya Kiswahili: Kabla ya Uhuru

Katika sehemu ifuatayo tutazungumzia kwa kifupi dhima za lugha ya Kiswahili na sababu za kukua na kuenea kwake kabla ya uhuru katika nchi za Afrika Mashariki. Kabla ya Uhuru; kuenea na umaarufu wake umechangiwa kwa kiasi kikubwa na mambo makuu manne tutayaja hapa kwa kifupi (kwa ufafanuzi zaidi tazama Massamba na wenzake 2012:14-22).

Kwanza ni: *Misafara ya kibiashara* baina ya wenyeji wenyewe na ile ya wafanyabiashara wa Kiarabu walioshughulika na biashara za pembe za ndovu na watumwa; wenyeji watumwa ambao walikuwa wapagazi ndio wanaotajwa katika kuenea huko kwa lugha hiyo.

Pili ni: *Dini*, hususan dini ya Kiislamu na ile ya Kikristo. Pamoja na biashara Waarabu waliitumia lugha hiyo kuwasilimisha au kutoa mafundisho au fasili ya kurani kwa lugha wanayoielewa wenyeji. Viongozi wa dini walianzisha maandishi ya Kiswahili yaliyotumia hati au alfabeti za Kiarabu. Vivyo hivyo Wamisionari walilazimika kukitumia Kiswahili katika shughuli zao za mahubiri, wakaanzisha shule za dini na wakatumia hati au alfabeti za Kirumi, ambazo zinatumika hadi hivi leo.

Tatu ni: *Ukoloni*, Katika vipindi vyote vya ukoloni juhudi mbalimbali zilichangia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Kwa mfano, katika kipindi cha ukoloni wa Kiarabu Kiswahili kilihimizwa kutumika kama lugha rasmi, katika maeneo kama madrasa na vyuo vya dini, na katika shughuli za tafsiri au fasili ya kurani. Katika kipindi cha ukoloni wa Kijerumani: Kiswahili kilitumika pia kama lugha ya mawasiliano na lugha ya kufundishia katika shule. Miongoni mwa wakoloni inatajwa kuwa wakoloni waliofuata baada ya Wajerumani yaani Waingereza, ndio waliofanya kazi kubwa zaidi katika kukikuza na kukieneza Kiswahili. Kwa maslahi na urahisi wa shughuli zao, Waingereza

walikuwa na azma ya kuwa na lugha moja ya kienyeji itakayotumika katika kufundishia katika nchi nne za Afrika Mashariki. Na hii inaturejesha katika historia ya usanifishaji ambapo mwaka 1925 Gavana wa iliyokuwa Tanganyika aliitisha mkutano wa wakuu wa elimu wa nchi hizo nne, na Lugha ya Kiswahili ndiyo iliyoonekana kuwa muafaka zaidi. Hii inaeleza sababu ya kuteuliwa kwake na haja ya kuteua lahaja mojawapo miongoni mwa lahaja zake nyingi ambayo ingesanifiwa na kutumika kama lahaja rasmi.

Sababu kuu ya nne iliyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili ni: *Harakati za Ukombozi*. Nchini Tanganyika na Kenya hasa, harakati za kisiasa za kujipatia uhuru zinatajwa kuwa na mchango mkubwa katika kupanua lugha ya Kiswahili katika matumizi. Kiswahili kilitumika kama lugha mawasiliano na chombo cha umoja. Mikutano yote kwa mfano ilifanyika kwa Kiswahili, nyimbo za kusifu chama cha TANU, na hata wito ukawa "Uhuru na Umoja". Hata hivyo Kiswahili kilifanikiwa na kupanuka zaidi nchini Tanganyika kuliko ilivyokuwa huko Kenya na Uganda, hali ambayo haijabadilika sana hata hivi leo.

**2.5 Dhima ya Kiswahili: Baada ya Uhuru na Sasa.**

Mara baada ya Uhuru Kiswahili kilikuwa sehemu muhimu ya utamaduni na silaha ya umoja hasa nchini Tanganyika na Kenya. Kiswahili kilipewa dhima ya lugha ya kufundishia masomo yote ila Kiingereza katika elimu ya msingi. Mnamo mwaka 1967, serikali ya Tanzania (baada ya Muungano na Zanzibar) ilikitangaza Kiswahili kama lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Zaidi vyombo na taasisi za ukuzaji na uenezaji wa lugha hiyo zikaundwa. Miongoni mwao ni Taasisi ya elimu ya watu wazima (mwaka 1963), Baraza la Kiswahili la Taifa, BAKITA ambacho ndicho chombo chenye wajibu mkubwa na mamlaka ya kisheria juu ya lugha ya Kiswahili hata sasa. Asasi nyingine muhimu ni kuipandisha hadhi ile kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Pia kuanzishwa kwa Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Idara hii ilikabidhiwa jukumu la kuifundisha na kukitumia Kiswahili chenyewe kama lugha ya kufundishia. Nchini Kenya Kiswahili kilianza kutumiaka bungeni mwaka 1975. Vile vile takriban vyuo vyote vilivyoundwa na serikali vinafundisha masomo ya Kiswahili kwa Kiswahili kufikia mwishoni mwa miaka ya 1980. Na juhudi muhimu zaidi nchini Kenya, ni kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika elimu ya msingi na sekondari (Massamba na wenzake 2012:25).

Katika miaka hii ya karibuni au zama hizi za utandawazi, Kiswahili kimeendelea kutanua wigo wake wa matumizi na kubeba dhima muhimu si tu Afrika Mashariki, bali nje ya Afrika Mashariki na hata duniani kwa ujumla. Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Tanzania na Kenya. Kiswahili ndiyo lugha ya mawasiliano mapana na lugha hii adhimu ina nafasi ya kipekee

katika masuala ya utamaduni kama tujuavyo lugha ni kielelezo cha utamaduni na vipengele vya utamaduni huakisiwa katika lugha yenyewe. Vilevile, kisiasa lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumika pote Afrika Mashariki na Kusini kuleta masikilizano ya kisiasa. Hivi karibuni lugha ya Kiswahili imeongezewa jukumu jipya la kuwa moja ya lugha rasmi ya shughuli za Umoja wa Afrika pamoja na zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bila kusahau kiuchumi, Kiswahili kinaendelea kutumika sana katika mawasiliano ya kibiashara kama ilivyokuwa tangu kale.

**2.6 Taaluma za Msingi katika Isimu ya Lugha**

Hapa tutafafanua viwango vya msingi vya Isimu ya lugha na kutolea mifano katika lugha ya Kiswahili pale inapojuzu. Kama msingi kwanza tutoe fasili ya dhana hizi mbili muhimu: *Isimu* na *Lugha*. Tukianza na *Isimu*, tunaweza kusema hii ni sayansi ya lugha: Isimu inachunguza na kudhihirisha kanuni za lugha wanazozitumia wazungumzaji wa lugha hiyo hata bila kufikiri. Besha (1994:9) anabainisha kuwa, "Lengo kuu la kwanza la taaluma ya isimu ni kuchambua na kuelezea maarifa aliyo nayo mjua lugha kuhusu lugha yake". Mekacha (2000:12) anataja vitengo vya isimu (taaluma inayofafanua miundo na uamilifu wa miundo hiyo katika lugha) kuwa ni vitano; fonetiki, fonojia, mofolojia, sintaksia na semantinki. Kwa upande wa Lugha: Kwa mujibu wa Massamba (2004:45) *Lugha* ni mfumo wa sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao. Lugha itumiayo maneno inaweza kugawanywa katika makundi mawili; lugha-unde na lugha asilia. Lugha ina dhima nyeti katika jamii inamotumika. Lugha ni kigezo cha kumfasili binadamu, ni nyenzo ya mawasiliano, ni nyenzo ya kumbukumbu, nyenzo ya kufundishia, kufikiri n.k (Mekacha 2000:12).

**2.6.1 Fonetiki na Fonojia** *(Phonetics & Phonology)*

*Fonetiki* na *Fonolojia* ni matawi mawili ya isimu yanayoshughulika na sauti za lugha katika lugha za binadamu. Matawi haya mawili ni tofauti lakini yenye uhusiano wa karibu pia. Hapa tutatolea ufafanuzi mfupi wa kila moja.

Tukianza na *Fonetiki*: "Fonetiki ni tawi ambalo hujishughulisha na uchunguzi na uchambuzi wa taratibu zote zinazohusiana na utoaji, utamkaji, usafirishaji, usikiaji na ufasili wa sauti za lugha za binadamu kwa jumla" (Massamba na wenzake 2004:5). Jambo la kusisitiza hapa ni kuwa Fonetiki hushughulika na sauti bila kujali lugha mahususi ambamo sauti hizo hutumika. Ndani ya tawi hili kuna matawi madogomadogo kadhaa, hapa tutataja manne tu. Tawi mojawapo ni *fonetiki-matamshi*, tawi hili dogo linachunguza namna ala sauti (yaani viungo vya matamshi) zinavyotumika katika matamshi ya sauti za lugha. Tawi la pili ni *fonetiki-akustika*; hili linashughulika na namna mawimbi sauti yanavyosafiri kutoka yanapotamkwa mpaka yanapomfikia msikilizaji. Tatu ni

*fonetiki-masikizi*; tawi hili linahusika na utambuzi wa sauti mbalimbali na uhusiano ulio baina ya sikio, neva za masikizi na ubongo. Nne ni *fonetiki- tibamatamshi*; tawi hili linashughulikia matatizo katika utamkaji wa sauti na utatuzi wake hasa kwa nia ya kuwasaidia watamkaji wenye matatizo hayo.

Kwa upande mwingine, *Fonojia* ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchunguzi, uchambuzi na uainishaji wa sauti ambazo hutumika katika mifumo mbalimbali ya sauti za lugha za binadamu (Massamba 2004:6). Tofauti na Fonetiki, Fonolojia hushughulika na sauti, mpangilio wake katika kuunda maneno yanayowakilisha maana, sambamba na kanuni na taratibu zinazoongoza mipangilio na mifuatano ya sauti hizo katika lugha fulani mahususi kama vile Kiswahili. Sauti za lugha hujulikana kama fonimu: yaani *irabu* na *konsonanti*. Kila lugha ina idadi maalum ya fonimu. Kiswahili kwa mfano kina jumla ya irabu 5 na konsonanti 26 (angalia Chomi 2013: 3). Massamba na wenzake (kashatajwa) anataja vipengele muhimu vya fonolojia ni kama vile; *Matamshi, Kiimbo, Mkazo, Lafudhi, Silabi* na *Otografia*. Kipacha (2005:40) naye anataja kuwa, taluma ya fonolojia ina matawi yake kadhaa miongoni mwao ni: Fonolojia vipande sauti, fonolojia arudhi, fonolojia zalishi, fonolojia leksika na fonolojia lugha alama.

### 2.6.2 Mofolojia *(Morphology)*

*Mofolojia* ambayo pia hujulikana kama *Sarufi Maumbo* ni utanzu mmojawapo wa Isimu (sarufi) ya lugha. Utanzu huu unahusu vipashio na taratibu ambazo huhusika katika uundaji wa maneno katika lugha (Kihore na wenzake 2001:15). Mofolojia hushughulika na namna ambavyo mofimu huungana na kuunda maneno katika lugha fulani. Chomi (2013:6-7) anabainisha mambo muhimu yanayoshughulikiwa katika taaluma hii, ikiwa ni pamoja na kueleza; maumbo (mofimu) ya maneno kwa ujumla (viambajengo vya maneno), dhana muhimu kama mofimu, neno, mzizi, kiambishi na alomofu, mbinu za kubaini mofimu na alomofu katika neno, aina na kazi za mofimu katika neno, mabadiliko ya kimofofonojia na kubaini kanuni za jumla zinazoongoza uundaji wa maneno. Kimofolojia, lugha ya Kiswahili inatambuliwa kuwa katika kundi la *lugha ambishi-bainishi (agglutinating language)*. Mkude (1995:8) anataja kuwa kwa kiasi kikubwa hii ni sifa ya lugha za Kibantu barani Afrika. Sifa ya lugha za aina hii ni kuwa, neno huundwa na mofimu kadhaa ambazo kila moja hubeba maana mahsusi.

### 2.6.3 Sintaksia *(Syntax)*

*Sintaksia* pia hujulikana kama *Sarufi Miundo* ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanguzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake (Massamba na wenzake 2012:34). Kila lugha ina kanuni au mpangilio wake wa maneno ili kupata tungo zinazokubalika

kwa mujibu wa taratibu za lugha hiyo. Kanuni hizi ni sehemu ya maarifa ya mjua lugha wa lugha husika. Viwango muhimu vya sintaksia au vipashio vinavyoshughulikiwa katika utanzu huu ni tungo na vipengele vyake yaani tungo; neno (aina za maneno), kirai, kishazi na sentensi. Kisintaksia Kiswahili kinawekwa katika kundi la lugha zenye muundo wa kitenzi katika nafasi ya katikati yaani "SVO" (yaani *Kiima- Kitenzi- Yambwa*). Hata hivyo Mkude (1995:9) anabainisha kwamba muundo huu unaweza kubadilika kutokana na haja/sababu mbalimbali ama za kisintaksia au za kisemantiki/pragmatiki katika mazungumzo ya kawaida.

### 2.6.4 Semantiki *(Semantics)*

Semantiki ni taaluma ya isimu inayojishughulisha na uchunguzi na uchambuzi wa maana za maneno au tungo katika lugha (Massamba 2004:75). Semantiki tunaweza kusema ndio moyo wa isimu, maana inatawala katika viwango mbalimbali vya lugha. Lugha kama tulivyokwisha kutangulia kusema, ni nyenzo ya mawasiliano, mawasiliano yanahusisha kubadilishana maana. Mada zinazoshughulikiwa zaidi na wanazuoni wa taaluma hii ni pamoja na maana ya maana, uhusiano wa maneno (ikiwa ni pamoja na; homonimu, homofoni, polisemia, haiponimia, sinonimia, homografia na antonimu) na tofauti kati ya dhima za kisemantiki (kwa ufafanuzi zaidi wa mada hizi tazama Kipacha 2005:92-105).

### 2.6.5 Taaluma nyingine

Pamoja na taaluma au viwango 5 vya msingi vilivyokwisha kutolewa ufafanuzi mfupi hapo awali, ni vyema tukataja hapa zipo taaluma nyingine anwai zinazojishughulisha na isimu ya lugha, matumizi ya lugha na jamii au uhusiano wa lugha na jamii zinamotumika lugha hizo. Taaluma hizo ni pamoja na pragmatiki (pragmatics), Isimutumizi (applied linguistics), Isimu-linganishi (Comparative linguisitics), Isimu Historia (Historical linguistics), na Isimujamii (Social linguistics). Nyanja kama isimujamii, na isimutumizi na isimulinganishi zinafundishwa kwa kiasi fulani katika kiwango cha chuo kikuu shahada ya awali na shahada za juu. Nyanja zingine bado hazijapata kuzungumziwa sana katika kazi za Kiswahili, kufundishwa au kujumuishwa katika mitaala katika ngazi ya Sekondari na hata vyuo vikuu katika shahada ya awali kwa ufahamu na uzoefu wa mwandishi.

## 3. Hitimisho

Makala hii imetalii na kutolea ufafanuzi mambo ya msingi kuhusiana na **Lugha ya Kiswahili** hapa tunatoa muhtasari wake. Kuhusu Lugha: Kwanza tumeelezea lugha ni nini na ina nafasi gani katika mawasiliano na utambulisho wa watu. Tukasisitiza kuwa hakuna jamii isiyo na lugha, kila

palipo na watu wana lugha yao. Na kuwa lugha na jamii havitenganishiki. Na hivyo basi ni muhimu kwa wajifunza lugha si tu kumudu stadi za lugha bali pia kujua utamaduni unaofungamana na lugha husika kwa lengo la kuwa na mawasiliano kamili. Pili, tumeangalia historia, asili na dhima ya Lugha ya Kiswahili kwa kifupi kabla na baada Uhuru wa Tanzania. Tatu, tumetambulisha taaluma za msingi za lugha hiyo kwa kutumia rejea kadhaa, maelezo na rejea hizo zinatarajiwa kumpa mwanga au mahali pa kuanzia mwanafunzi mgeni au mtu yeyote mwenye raghba ya kujua kuhusu asili, historia, dhima ya lugha ya Kiswahili au kumakinikia katika taaluma fulani ya Isimu ya Lugha.

Makala hii ni mwendelezo wa juhudi za mwandishi kuangazia vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Kiswahili ya kama sehemu ya kutajirisha maarifa juu ya Utamaduni wa Kiswahili hususan kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hata hivyo bado tunaendelea kutoa wito wa kuongeza rejea zaidi kwa vipengele vingine vya Lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa haja ya kukidhi haja ya wajifunzaji wa Lugha hii kama lugha ya kigeni. Miongoni mwa vipengele vinavyopendekezwa kuangaziwa zaidi katika kazi zijazo ni pamoja na; mambo ya fasihi ya Kiswahili/Kiafrika, sanaa na burudani.

## Marejeo

Besha, Ruth Mfumbwa

2007 Utangulizi wa Lugha na Isimu (Chapa ya Pili), Macmillan AidanLtd, Dar es Salaam.

Bosha, I.

2000 Taathira za Kiarabu Katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Isack, Zainabu Kassu

2018 “Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika *Frontier of Foreign Language Education 1*, *105-118*.

2019 “Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika *Frontier of Foreign Language Education 2*, *259-269*.

2020 "Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi", katika *Frontier of Foreign Language Education 3*, *193-205*.

2021 "Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili", katika *Frontier of Foreign Language Education 4*, *223-233*.

TUKI

2013 Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 3), Oxford University Press, Nairobi.

Kihore, Y.M na wenzake

2001 Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo, TUKI, Dar es Salaam.

Kipacha Ahmad

2005 Utangulizi wa Lugha na Isimu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B na wenzake

2004　Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo, TUKI, Dar es Salaam.

2012　Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo (Chapa ya Nne), TUKI, Dar es Salaam.

Massamba, David P.B

2004　Kamusi ya isimu na Falsafa ya Lugha, TUKI, Dar es Salaam.

2012　Misingi ya Fonojia, TUKI, Dar es Salaam.

Mbaabu Ireri

2007　Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili, TUKI, Dar es Salaam.

Mekacha, Rugatiri D.K

2000　Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili, Osaka University of Foreign Studies, Japan.

Mkude, Daniel J.

1995　Towards a Semantic Typology of The Swahili Language, ILCAA, Tokyo.

Wesana-Chomi, E.

2013　Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili, TATAKI, Dar es Salaam.